

HALMASHAURI YA WILAYA YA ARUSHA

(Barua zote za kiofisi zitumwe kwa Mkurugenzi Mtendaji)

Mkoa wa Arusha,
Telegram: Arusha.
Simu: 073 6500476,
Faksi: 250 3701.
Email:ded@arushadistrict.go.tz



Ukumbi wa Wilaya,
S. L. P. 2330,
ARUSHA.

www.arushadc.go.tz.

MIRADI INAYOTEKELEZWA KATIKA HALMASHAURI YA ARUSHA KWA MWAKA WA FEDHA 2016/2017

Halmashauri ya Arusha kwa mwaka wa fedha 2016/2017 inatekeleza miradi mbalimbali katika kata zote 27 za Halmashauri kwenye sekta za Elimu, Afya, Maji, Miundombinu ya Barabara, Mazingira, Kilimo, Mifugo, Ardhi, Maliasili na Mipangomiji.

Katika kuhakikisha huduma za jamii zinapatika kwa urahi kwa kuwa na uwiano sawa wa maneo ya miji na vijiji, Halmashauri imejikita kuelekeza nguvu katika kutekeleza miradi katika kata zote kwa kuzingatia zaidi vipaumbele na uhitaji wa huduma wa wananchi wa eneo husika.

Kwa mwaka wa fedha 2016/2017 Halmashauri inatekeleza miradi mipya kwa mwaka huu wa fedha pamoja na miradi bakaa inayoendelea kutoka mwaka wa fedha uliopita wa 2015/2016.

Kadhalika halmashauri inatekeleza miradi yake kwa kuzingatia zaidi ushirikishwaji wa wananchi, Seriklali pamoja na wadau mbalimbali wa maendeleo wa ndani na nje ya Tanzania.

Halmashauri pia inahakikisha miradi hiyo inazingatia weledi ikiwemo usimamizi thabiti wa matumizi ya fedha na utekelezaji unaozingatia thamani halisi ya fedha kwa kulinganisha na ubora wa mradi 'value for money'.

Miradi inayotekelezwa ni miradi ya Ujenzi na Ukarabati wa Vyumba vya Madarasa, Nyumba za walimu, Bwalo, Mabweni pamoja na vyoo vya wanafunzi katika shule za Msingi na Sekondari, Ujenzi na Ukarabati wa Zahanati, Vituo vya Afya na Hospitali pamoja na ujenzi wa nyumba za wahudumu wa Afya ikiwemo madaktari na wauguzi, Ujenzi na Ukarabati wa miundombinu ya barabara pamoja na vivuko, madaraja na mitaro ya kupitisha maji kwenye kingo za barabara, Ujenzi wa Skimu za Umwagiliaji, ujenzi wa miundombinu ya Maji, ujenzi wa majosho na machinjio pamoja na uhifadhi wa ardhi na utunzaji wa mazingira.

Picha zifuatazo zimejikita kuonyesha hali halisi ya muonekano wa Miradi inayotekelezwa kwa mwaka wa fedha 2016/2017: -

1. UJENZI WA VYUMBA VYA MADARASA SHULE YA MSINGI MUSA.

Mradi wa ujenzi wa vyumba viwili vya madarasa na ofisi ya walimu shule ya Msingi Musa kata ya Musa huo mpaka sasa umegharimu kiasi cha **Tsh. 16,500,000.00** Ikiwa **Tsh. 9,000,000.00** fedha za *Own Source*, **7,500,000.00** fedha za Lakilaki na bado unahitaji kiasi cha **Tsh. 15,200,000.00** kwa ajili ya umaliziaji wa jengo hilo.



2. UJENZI WA CHOO SHULE YA MSINGI MOIVO.

Ujenzi wa choo cha matundu 10 shule ya Msingi Moivo kata ya Moivo umeghalimu kiasi cha Tsh. 12,684,000.00 fedha za lakilaki.



3. UKARABARI WA VYUMBA VYA MADARASA SHULE YA SEKONDARI MATEVESI.

Ukarabati wa vyumba viwili vya madarasa shule ya Sekondari Matevesi kata ya Matevesi kwa kusakafia kwa vigae (tiles) na kupaka rangi ndani na nje, ukarabati umeghalimu kiasi cha Tsh. 8,000,000.00 ikiwa ni fedha za Lakilaki.



4. VYUMBA VYA MADARASA SHULE YA SEKONDARI SAMBASHA.

Ujenzi wa vyumba viwili vya madarasa na ofisi ya walimu shule ya Sekondari Sambasha kata ya Sambasha umeghalimu kiasi cha Tsh. 30,000,000.00 kutoka vyanzo mbalimbali vya fedha ikiwemo Tsh. 20,000,000.00 fedha za CDG Tsh. 10,000,000.00 na fedha za Lakilaki.



5. UJENZI WA CHUMBA KIMOJA CHA DARASA SHULE YA SEKONDARI SAMBASHA.

Ujenzi wa chumba kimoja cha darasa shule ya Sekondari Sambasha kata ya Sambashaujenzi umeghalimu kiasi cha **Tsh. 17,000,000.00** darasa lililojengwa kwa nguvu za wananchi wa kijiji cha Sambasha katika kuchangia maendeleo ya Elimu katika kata yao.



6. HOSTELI YA WANANFUNZI CHUO CHA UFUNDI MWANDETI.

Ujenzi wa vyumba Hosteli ya wananfuzni chuo cha Ufundi Mwandeti kata ya Mwandeti. Hosteli hii imetengewa kiasi cha Tsh. 30,000,000.00 ikiwa ni fedha za Lakilaki.



7. VYUMBA VYA MADARASA SHULE YA SEKONDARI SOKONI II.

Kuongezea ujenzi wa vyumba 10 vya madarasa na ofisi za walimu ghorofa 2 katikashule ya Sekondari Sokoni II kata ya Sokoni II. Ujenzi utagharimu kiasi cha **Tsh. 201,000,000.00** mpaka sasa kimetumika kiasi cha **Tsh. 150,416,100.00** kutoka vyanzo mbalimbali vya fedha ikiwemo, Nguvu za wananchi **Tsh. 7,570,000.00**, Mchango wa Wazazi **Tsh. 19,846,100.00**. Halmashauri imetoa kiasi cha **Tsh. 123,000,000.00**, awamu ya kwanza ilitoa **Tsh. 85,000,000.00** fedha za **CDG**, ikaota tena kiasi cha **Tsh. 20,000,000.00** fedha za **CDG**, mapato ya ndani **Tsh. 6,000,000.00** na **Tsh. 12,000,000.00** fedha za Lakilaki.



8. VYUMBA VYA MADARASA NA CHOO SHULE YA MSINGI THEMIYASIMBA.

Huu ni moja ya miradi inayotekelezwa na TASAF awamu ya III katika kujenga na kuboresha mioundombinu inayolenga sekta za Elimu. Katika shule ya Msingi Themiyasimba kata ya Bwawani, TASAF inatekeleza miradi miwili mradi waUjenzi wa vyumba viwili vya madarasa, Ofisi ya walimu na ujenzi choo chenye matundu sita kwa gharama ya **Tsh.84,789,886.00** ikiwa TASAF imegaramia kiasi cha **Tsh. 71,760,886.00**, Halmashauri imechangia kiasi cha **Tsh. 5,507,000.00** na Jamii wananchi wa kaijiji cha Themiyasimba wamechangia nguvu kazi ambayo imethaminishwa na kiasi fedha **Tsh. 7, 522,000.00**.



9. UJENZI WA CHOO SHULE YA MSINGI THEMIYASIMBA.

Ujenzi wa choo cha matundo sita shule ya Msingi Themiyasimba uko katika hatua za awali, Mradi unaotekelezwa na TASAF awamu ya III.



10. UJENZI WA MADARASA SHULE YA MSINGI OLOKII.

Ujenzi wa vyumba viwili vya madarasa shule ya Msingi Olokii kata ya Bwawani



11. UJENZI WA DARASA SHULE YA MSINGI LEMUGURU.

Ujenzi wa vyumba vya madarasa shule ya Msingi Lemugur kata ya Matevesi mradi umepangiwa kiasi cha **Tsh. 8,000,000.00** fedha za mgao wa Lakilaki kama inavyoonekana katika picha mradi uko katika hatua za awali.



12. MRADI WA UHIFADHI WA ARDHI NA UDONGO LEMUGUR.

Mradi wa Uhifadhi wa Ardhi na udongo kijiji cha Lemugur ni moja ya Miradi inayotekelezwa na TASAF awamu ya III. Mradi huu unatekelezwa kwa kutoa ajira ya muda kwa jamii ambapo walengwa wa Mpango wa Kususuru kaya Masikini hufanyakazi na kulipwa ujira wa **Tsh. 2,300.00** kwa siku.

Mradi huu unathamamni ya **Tsh. 70,545,814.00** fedha ambazo asilimia **50%** inatumika kugharamia mahitaji ya mradi na asilimia **50%** inatumika kulipa ujira kwa walengwa wa kaya masikini.

Katika Kijiji cha Lemugur itaoteshwa jumla ya miti 10,000 pamoja na kuhifadhi ardhi kwa kuweka makinga maji.



13. UKARABATI WA BWENI SHULE YA SEKONDARI OLJORO KATA YA LAROI.

Ukarabati wa jengo la Hosteli ya wanafunzi shule ya Sekondari Oljoropamoja na kuweka uzio kwa gharama ya Tsh. 10,000,000.00 fedha za mgao wa Lakilaki.



14. UJENZI WA CHUMBA CHA DARASA SHULE YA MSINGI THEMIYASIMBA.

Ujenzi wa chumba cha darasa shule ya msingi Themiyasimba kata ya Bwawani uko kwenye hatua za umalizia Halmashauri imetoa kiasi cha **Tsh.8,000,000.00** fedha za mgao wa **Lakilaki** kwa ajili ya kupaua.



15. BWENI LA WANAFUNZI SHULE YA SEKONDARI MLANGARINI.



17. UJENZI WA MADARASA SHULE YA SEKONDARI MLANGARINI.

Ujenzi wa madarasa mawili ya kidato cha V shule ya sekondari Mlangarini kata ya Mlangarini halmashauri imetenga kiasi cha Tsh.20,000,000.00 fedha za mgao wa Lakilaki.



18. MRADI WA UHIFADHI WA ARDHI NA UDONGO THEMİYASIMBA.

Mradi wa Uhifadhi wa Ardhi na udongo kijiji cha Themiyasimba ni moja ya Miradi inayotekelezwa na TASAF awamu ya III. Mradi huu unatekelezwa kwa kutoa ajira ya muda kwa jamii ambapo walengwa wa Mpango wa Kususuru kaya Masikini hufanyakazi na kulipwa ujira wa Tsh. 2,300.00 kwa siku.

Mradi huu unathamamni ya Tsh. 70,545,814.00 fedha ambazo asilimia 50% inatumika kugharamia mahitaji ya mradi na asilimia 50% inatumika kulipa ujira kwa walengwa wa kaya masikini.



19. UJENZI WA NYUMBA YA WALIMU SHULE YA MSINGI LAROI.

Ujenzi wa nyumba ya walimu yenye sehemu mbili (2in 1) shule ya Msingi Laroi kata ya Laroi, huu ni moja ya miradi ya TASAF awamu ya III inayotekelezwa katika kujenga na kuboresha mioundombinu inayolenga sekta za Elimu. Mradi huu umegarimu kiasi cha **Tsh.84,789,886.00** ikiwa TASAF **Tsh. 71,760,886.00**, Halmashauri imechangia kiasi cha **Tsh.5,507,000.00** pamoja na wananchi wa kijiji cha Laroi waliofanya kazi ya kuchimba msingi, kukusanya mawe na kuleta vifaa vya kufanyia kazi iliyothaminihwa kwa fedha kisi cha **Tsh. 7,522,000.00** . Hatua za utekelezaji wa mradi wa ujenzi huo.



20. UJENZI WA NYUMBA YA WATUMISHI WA AFYA ZAHANATI YA THEMIYASIMBA

Ujenzi wa nyumba ya watumishi wa Afya Zahanati ya Themiyasimba yenye sehemu mbili (2 in 1) ni mradi unaoedelea kutekelezwa kwa mwaka huu wa fedha umepewa kiasi cha **Tsh. 15,000,000.00** fedha za LCDG.



21. UJENZI WA BWALO LA CHAKULA SHULE YA SEKONDARI MWANDETI.

Ujenzi wa Bwalo la kulia chakula shule ya Sekondari Mwandeti kata ya Mwandeti ni mradi



22.UJENZI WA JINGO LA OFISI YA WALIMU SHULE YA SEKONDARI EINOTI

Umaliziaji wa jengo la Ofisi ya walimu shule ya Sekondari Einoti kata ya Kisongo mradi uliogharimu kiasi cha **Tsh. 12,000,000.00**fedha za mgao wa Lakilaki.



23.UJENZI WA KITUO CHA AFYA ENGORORA.

Ujenzi wa Kituo cha Afya Engorora jingo limejengwa kwa nguvu za wananchi kwa kushirikiana na wadau mbalimbali wa maendeleo wa kijiji cha Engorora.



24. UJENZI WA ZAHANATI ILKERINI.

Ujenzi wa Zahanati ya Ilkerini kata ya Kisongo mradi ambao halmashauri imetoa kiasi cha Tsh.15,000,000.00 fedha za LCDG kwa ajili ya umaliziaji wa jingo hilo.



25. UKARABATI WA CHUMBA CHA WAZAZI KITUO CHA AFYA OLKOKOLA.

Ukarabati wa kituo cha Afya Olkokola kata ya Lemanyata Halmashauri imetoa kiasi cha Tsh. 15,000,000.00 fedha za LCDG kwa ajili ya kutengeneza chumba cha upasuaji (Theater) na kiasi cha Tsh. 4,100,000.00 fedha za Mfuko wa Jimbo kwa ajili ya kutengeneza miundombinu ya umeme na kuunganisha umeme kwenye kituo hicho cha Afya.



26.

26. UJENZI WA MIFEREJI YA KINGO ZA BARABARA YA NGARAMTONI - SELIANI HOSPITAL-LONGING'O.

Mradi mpya wa ujenzi wa mifereji kwenye kingo za Barabara ya Ngaramtoni - Seliani Hospital-Longing'o. Mifereji hiyo imejengwa urefu wa mita 300 ikiwa mita 150 kila upande mradi umegharimu kiasi cha Tsh..... Mifereji hiyo itaendelea kujengwa kadri fedha zitakavukuwa zinapatikana.



27.Mradi wa Maji Ngaramtoni



28. Ujenzi wa choo shule ya msingi Oltrumet

Ujenzi wa choo shule ya Msingi Oltururmet kata ya Oltururmet uko katika hatua za awali na Halmashauri imepeleka kiasi cha Tsh. 10,000,000.00 kutoka kwenye fedha za Maendeleo.



29. UKARABATI WA MADARASA SHULE YA SEKONDARI OLTUROTO

Ukarabati wa vyumba vine vya madarasa shule ya sekondari Olturoto kata ya Olturoto ukarabati huo utajumuisha kubadilisha sakafu na kuweka sakafu ya vigae 'tiles' na kupaka rangi ndani na nje.



30. UJENZI WA NYUMBA YA WATUMISHI WA AFYA ZAHANATI YA IMBIBIA.

Ujenzi wa nyumba ya wahudumu wa Afya katika Zahanati ya Imbibia kata ya Mwandeti yenye sehemu mbili (2 in 1) imetengewa kiasi cha Tsh. 15,000,000.00 fedha LCDG.

